



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS -IKULU**

**HOTUBA YA KATIBU MKUU KIONGOZI MHE. BALOZI HUSSEIN A.  
KATTANGA KATIKA SEMINA MAALUM NA MAKATIBU WAKUU YA  
KUJADILI UMUHIMU NA MCHANGO WA BIMA KATIKA UCHUMI WA  
NCHI -INAYOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA KAMBARAGE WA WIZARA  
YA FEDHA NA MIPANGO JIJINI DODOMA SEPTEMBER 16, 2022.**

- 1. Ndugu Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar,**
- 2. Kamishna wa Bima,**
- 3. Wakurugenzi wote wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Nchini,**
- 4. Washiriki wa Semina na Wageni waalikwa wote;**

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

1. Napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma kwa kutuwezesha kufika hapa tukiwa na afya njema na kutupa nafasi ya kukusanyika mahali hapa katika semina maalum na adhimu cha Makatibu Wakuu na Kamishna wa Bima.
2. Kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru na kuwapongeza viongozi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania, kwanza kwa kuona umuhimu wa kufanyika kwa semina hii, lakini pili kuhakikisha wanaishauri serikali kuhusu kuhakikisha shughuli za wananchi kijamii na kiuchumi zinakingwa na sekta ya Bima. Jitihada hizi zina malengo ya kuhakikisha ustawi endelevu wa uchumi kwa mustakabali bora wa wananchi wetu na vizazi vyetu vijavyo.

**Ndugu Makatibu Wakuu,**

3. Sekta ya Bima ni moja ya sekta muhimu sana katika uchumi wa nchi, ni sehemu muhimu ya Sekta ya Fedha ambayo inalinda mustakabali wa biashara na uchumi kwa ujumla. Uchumi imara hutegemea sekta ya fedha iliyo Madhubuti na yenye udhibiti makini ili kuilinda nchi dhidi ya majanga ya kifedha.

Watu wengi hudhani kuwa majukumu ya Sekta ya Bima huishia katika kutoa ulinzi dhidi ya masuala ya kifedha, kupoteza mali au uwezo wa kupata mapato na mengineyo mengi. Ingawa hayo yote ni muhimu na sahihi, sekta ya Bima ina mchango mkubwa katika ukuaji na maendeleo ya uchumi wa kisasa. Maeneo hayo ni Pamoja na ulinzi/usalama wa sekta ya fedha, utulivu wa

kiuchumi/kifedha ikiwa ni Pamoja na kulinda mitaji na kuleta maendeleo. Makampuni ya Bima mionganini mwa wawekezaji wakubwa duniani.

Kimsingi, Sekta ya Bima inapaswa kuchangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi wa taifa letu kwa kutoa utulivu katika utendaji wa Biashara na kuzalisha rasilimali fedha za muda mrefu kwa ajili ya miradi mbalimbali. Aidha, Sekta ya Bima inapaswa kushiriki kikamilifu katika uwekezaji, kupunguza hasara, uthabiti wa kifedha na kukuza shughuli za biashara kwa maendeleo endelevu.

4. Serikali ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua hayo na imedhamiria kuleta maendeleo kwa wananchi kwa kufanya mageuzi makubwa katika sekta zote za uchumi nchini. Serikali ina dhamira ya dhati ya kukuza uchumi na kuleta maendeleo ya wananchi wake, kwa kuvutia wawekezaji na kupunguza urasimu katika taratibu za uwekezaji. Katika kutekeleza azma hiyo, shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii zinazoendelea nchini zitahitaji sekta ya Bima iliyo imara ili kuhakikisha maendeleo yetu ya kiuchumi yanalindwa.
5. Ili kutoa msukumo katika kukuza uchumi, Serikali imekua ikiandaa Sera, Sheria, kanuni, maelekezo na mipango mbalimbali inayoweka misingi madhubuti kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla ikiwa ni pamoja na sekta ya Bima. Kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi Sura ya Pili, kipengele cha 20(b); 37(h na i) na 83(e) Serikali imepewa jukumu la kuimarisha huduma za Bima, kuweka misingi imara itakayowezesha kukua kwa huduma za Bima nchini na kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa Bima wa wananchi wengi ikiwa ni pamoja na Bima ya afya kwa wote. Aidha, Mheshimiwa Rais kuitia hotoba aliyoitoa wakati akilihutubia Bunge la 12 mwezi April, 2021 aliekeleza kwamba suala la Bima ya kilimo na Bima ya afya kwa wote liangaliwe kwa karibu zaidi.

## Ndugu Makatibu Wakuu,

6. Vilevile, kupitia Sheria mbalimbali, Serikali imekuwa ikijenga utaratibu wa matumizi ya Bima katika Uchumi. Sheria ya Bima na Sheria ya Usalama Barabarani, Mwaka 2017, Serikali kupitia Sheria No. 7 ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali ilianisha maeneo yafuatayo katika kuhakikisha shughuli zote za uchumi zinakingwa na Bima. Maeneo hayo ni;

- a. Sheria ya Madini SURA. 123.

Kupitia mabadiliko hayo, **Vifungu Namba 102, Kifungu kidogo cha 4a na 106 Kifungu kidogo cha 2e**, vimeelekeza kutumika kwa huduma za Bima kutoka kampuni za ndani katika shughuli tajwa za madini ili kukidhi matakwa ya leseni.

- b. Sheria ya Usimamizi wa Mazingira SURA. 191.

Sheria **kupitia kifungu Na. 109 kifungu kidogo cha 2c**, imetoa uwezekano wa kutumia huduma za Bima ili kukinga watu dhidi ya majanga na kupunguza athari kipindi majanga yanapoweza kutokea.

- c. Sheria ya Bima SURA 394.

Mabadiliko ya Sheria hii yaligusa vifungu vitatu, lakini kutokana na umuhimu wa kikao kazi hiki naomba niwakumbushe kidogo **Kifungu Na. 133, Kifungu kidogo cha (1-3)** kinachotaka majanga yote yanayotokana na shughuli za uchumi nchini kukatiwa Bima na kampuni za Bima zilizosajiliwa nchini. Pia, bidhaa zote zinazoingizwa nchini kwa njia ya maji, anga na nchi kavu ikiwa zitahitaji Bima lazima iwe imekatwa kupitia kampuni za Bima zilizo na usajili nchini.

Aidha, hivi karibuni Serikali kupitia Sheria ya Fedha Na. 05 ya Mwaka 2022 imeainisha maeneo muhimu manne ili kuongeza wigo wa Bima za lazima (mandatory insurance) kwa kujumuisha masoko ya umma, majengo ya biashara, bidhaa zote zinazoagizwa kutoka nje, vyombo vyaa baharini na vivuko. Hatua ambayo inalenga kuimarisha ushirikishwaji wa kifedha (financial inclusion) na kuongeza matumizi ya Bima nchini.

Ni Imani yangu kuwa mabadiliko haya ya sheria yatachochea ukuaji wa soko la ndani la Bima kwani pamoja na takwimu za miaka sita yaani kuanzia mwaka 2016-2021, kuonyesha kuwa soko letu limekuwa na wastani wa ukuaji wa asilimia 7% bado ukuaji huu haujaendana na mchango wa sekta hii muhimu katika pato la taifa;

**Ndugu Makatibu Wakuu,**

7. Kwa kuwa masuala ya Bima ni mtambuka na yanaunganisha sekta zote za kiuchumi na kijamii katika sekta ya Umma na Binafsi, ni vema yakashughulikiwa kwa pamoja badala ya kuiachia Wizara au Taasisi moja tu. Aidha, Idara za Serikali zinazosimamia Bima, zina jukumu la kusimamia mwenendo wa soko la Bima. Hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa *sectoral coordination*, semina hii isitumike kusambaza elimu ya Bima pekee, bali kuzileta pamoja Wizara na Taasisi za Umma kwa ajili ya jambo moja, uratibu wa pamoja na utekelezaji wa pamoja. Utaratibu huu ni mzuri na unapaswa kuzingatiwa kwa ajili ya kushughulikia masuala yote mtambuka.

**Ndugu Makatibu Wakuu,**

8. Serikali imeipa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima malengo mbalimbali ya kukuza sekta ya Bima ili kufanikisha azma ya kulinda shughuli za wananchi kiuchumi na kijamii. Lakini pia, kuhakikisha soko la Bima nchini linakuwa sehemu salama na ya kuaminika kwa wananchi na wawekezaji. Hivyo, kupitia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mpango Mkuu wa Kuendeleza Seka ya Fedha Nchini, Mamlaka imepewa wajibu wa kutekeleza yafuatavyo:
  - a. Kuhakikisha asilimia 50 ya Watanzania wenyе umri wa kuanzia miaka 18 wanapata huduma za huduma mbalimbali za Bima ifikapo mwaka 2030 (Tofauti na sasa ambapo ni asilimia 16 tu ya Watanzania wanatumia huduma za biam Nchini)
  - b. Kuhakikisha elimu ya Bima inawafakia Watanzania wengi zaidi na kipimo kilichowekwa kwenye mipango yetu ni kuwafikia watanzania takribani asilimia 80 ifikapo mwaka 2030 tofauti na asilimia 36 tu ya sasa.

- c. Kuhakikisha idadi ya watanzania wenyе Bima za maisha inaongezeka;
- d. Kuhakikisha 10% ya tozo za Bima zinatokana na shughuli za kilimo;
- e. Kuhakikisha sekta ya Bima inatoa na kutengeneza ajira kwa vijana;
- f. Kuhakikisha mifumo ya TEHAMA katika sekta ya Bima inakuwa rafiki na kuwiana na mifumo mingine ya sekta ya fedha.

**Ndugu Makatibu Wakuu,**

- 9. Nimejulishwa kuwa Mamlaka ya usimamizi wa Bima kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango imeandaa na kusambaza miongozo mbalimbali ya Bima yenyе lengo la kuendeleza soko la Bima. Miongozo hiyo ni; Mwongozo wa Maafisa Wauza Bima, Mwongozo wa Uuzaji Bima Kidijitali, Mwongozo wa Takaful na Mwongozo wa utoaji taarifa za mahesabu. Miongozo hii inalenga kuchochea upatikanaji wa huduma za Bima kwa wananchi na pia kuongeza ajira kwa vijana wetu. Hivyo, tuitumie ipasavyo.

**Ndugu Makatibu Wakuu;**

- 10. Kwa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan imedhamiria kutumia rasilimali zilizopo nchini ili kuboresha na kuinua uchumi wa nchi na mwananchi mmoja mmoja, hatuna budi kuendelea kushirikiana ili kulisukuma gurudumu hili kwa kuhakikisha shughuli zote za kiuchumi na kijamii zinakingwa na sekta hii ya Bima.
- 11. Hapa Tanzania, Sekta ya Bima ni huria ambapo Serikali pia inafanya biashara hiyo. Ili kufikia malengo tarajija, Wizara ya Fedha na Mipango kupitia taasisi za Bima ina jukumu la kuongeza wigo wa Bima na kufikia watu wengi zaidi. Aidha, Serikali lazima ijipange kuingia katika maeneo muhimu ya Serikali ambayo yanahitaji utulivu wa kifedha kama vile pensheni ya watumishi wa Serikali na afya ya wananchi. Tutumie Sekta ya Bima katika kukuza na kuendeleza maeneo nyeti na yenyе umuhimu kwa Serikali kama vile makazi, shule na hospitali au Bima za mazao n.k.

Cha kuzingatia ni kutumia Sekta ya Bima katika kukuza uchumi na kulinda uchumi ikiwa ni Pamoja na kuzuia uhamishaji wa mitaji (capital flights). Kwa msingi huo, udhibiti wa Sekta ya Bima ni muhimu. Bila udhibiti makini, nchi yetu inaweza kutawaliwa kiuchumi. Hivyo, kuna umuhimu mkubwa wa kujenga sekta Madhubuti ya Bima.

12. Naielekeza Mamlaka ya usimamizi wa Bima kutekeleza majukumu yao na mipango yao waliyojiwekea kwa umakini na weledi mkubwa. Hii ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa sheria ya Bima namba 10 ya mwaka 2009 na Sheria ya Fedha namba 5 ya mwaka 2022 inayoelekeza kuwepo kwa Bima za lazima (mandatory insurance) kwa kujumuisha Bima za masoko ya umma, majengo ya biashara, bidhaa zote zinazoagizwa kutoka nje, vyombo vya bahrini na vivuko. Aidha, Serikali itahakikisha kuwa Taasisi zake zinazolinda uchumi wa Taifa zinatekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija.

**Ndugu Makatibu Wakuu;**

13. Nimejulishwa kuwa kutakuwa na mawasilisho mahsus kuhusu uendeshaji wa soko la Bima na tutapewa uzoefu kutoka Uganda na Uingereza Pamoja na kutapata nafasi ya kusikiliza wasilisho kutoka kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania. Aidha, washiriki watapata nafasi ya kujadili mawasilisho hayo.
14. Kwa hayo machache ninatamka kwamba Semina ya Makatibu Wakuu Kuhusu Mchango wa Sekta ya Bima katika Uchumi wa Nchi imefunguliwa Rasmi. Nawatakia kila la Kheri.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.**